

7

SHULE YA KANYAMEDHA MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA KWANZA KISWAHILI



JINA:

NAMBARI YA USAJILI:

DARASA:

A. KUSOMA UFAHAMU [Alama 8]

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 1 hadi 5

MAWAZO YA OLUDHE

Oludhe aliketi kwenye roshani ya jumba lake huku ameshika tama. Ungemtazama kutoka mbali ungeona mja aliyevunjikiwa kabisa. Ubongo wa bwana huyu ulikuwa umefurika mawazo ambayo yalitishia kuupasua.

“Kweli mimi ndimi yule mja ambaye marehemu baba yangu alizoea kusema kwamba huchomwa vidole na sima ambayo imelala nje usiku kucha. Na yawe mapenzi ya Mwenyezi Mungu, lakini... Binti wa ngapi huyu? Itakuwaje hata baada ya Beth kurudi kwao kwa kosa hili, Anita naye pia afuate kisogo chake? Kwa nini wake wangu wanaidhalilisha kiasi hiki? Sina pa kuuweka uso mbele ya wazee wenzangu. Mali hii yote atairithi nani?” Oludhe alijisemea na kujiuliza maswali mfululizo.

Hata alipokuwa akijiuliza maswali haya, Oludhe alijua kwamba kitoto hiki kilichokuwa kikimlilia ndicho kilichokuwa kitindamimba cha mkewe, Anita. Chenyewe kilikuwa cha tano, akiongezea wale watatu wa Beth. Hata alipopiga hesabu akilini mwake, Oludhe alifahamu fika kwamba hapakuwa na matumaini ya hali yake kupata afueni.

“Tabibu mwenyewe amesema kwamba itakuwa hatari kwa mke wangu kupata mtoto mwingine. Alikuwa katuonya hata hapo awali lakini ilibidi nimlazimishe Anita ajaribu tena. Matokeo ndiyo haya.” Oludhe alijisemea huku akitikisa kichwa na kuendelea kujizungumzia kwa sauti.

“Ningekuwa sina elimu na mali hii yote, ningefurahia kuwa na hao mabinti. Ningewaoza kama wafanyavyo wazee wengine. Hata huyu Lulu wa Beth singemwelimisha hadi chuo kikuu. Angepata mchumba na kuanza Maisha ya ndoa kama wengine wa rika lake hata kabla ya kukamilisha shule ya msingi. Ndivyo ilivyo desturi yetu huku. Hata hivyo, sina haja ya mahari wala zawadi kutoka kwa mkwe yeyote. Nilichotamani ni mwana wa kuliendeleza jina langu. Sasa ulimwengu umeninyima haya yote. Inabidi niendeleo kufuja mali yangu kuwaelimisha wapita njia. Laiti hata ningekuwa na simba mmoja tu wa kunipangusa machozi!” Oludhe aliendelea kulalamika zaidi.

Akiwa katika hali hii, hakumwoma binti yake Dolly ambaye alikuwa amekuja kumletea chai ya jioni. Hata Dolly alipomwita kwa sauti yenye upole wa njiwa, Oludhe aliomba kwamba mtoto huyu asije akawa ametambua yale ambayo alikuwa akiwazia. Alijua kwamba hili lingeuatua moyo wa binti huyu ambaye alimpenda kama mboni ya jicho lake.

MASWALI

1. Oludhe alikuwa ameketi wapi?

[Alama 1]

.....
.....

2. Kwa nini Oludhe alikuwa na mawazo mengi?

[Alama 1]

.....
.....

3. Oludhe alikuwa na watoto wangapi? [Alama 1]

.....
.....

4. Taja wahusika watano waliotajwa katika hadithi hii [Alama 5]

.....
.....
.....
.....

5. Jamii ya Oludhe inaendeleza unyanyasaji wa kijinsia. Thibitisha hoja hii. [Alama 1]

.....
.....

FASIHI [ALAMA 10]

Soma nyimbo zifuatazo kisha uyajibu maswali yafuatayo

NYAMAZA KIPENZI

*Nyamaza kipenzi changu, tulia
Mama anainjika chungu, tulia
Ukilia unanipa machungu, tulia
Ewe kichanga changu, tulia
Tulia eeh, tulia aaah
Tulia eeh, tulia aaah*

NAPAKA RANGI

*Napaka rangi michoro yangu
Napaka rangi michoro yangu
Niangalie, niangalie
Waweza kufanya nifanyavyo?
Waweza kufanya nifanyavyo?*

1. Nyimbo zifuatazo ni za aina gani? [Alama 2]

a) Nyamaza kipenzi-

.....

b) Napaka rangi-

.....

2. Taja sifa tatu za wimbo “**NYAMAZA KIPENZI**” [Alama 3]

.....
.....
.....

3. Taja sifa tatu za wimbo “**NAPAKA RANGI**” [Alama 3]

.....
.....
.....

4. Taja tanzu mbili kuu za fashi

[Alama 2]

SARUFI [ALAMA 20]

Kutoka swali la 1 hadi 4 toa jibu sahihi.

1. Andika maneno mawili yenye sauti /th/ na mwawili yenye sauti /dh/

[Alama 4]

.....

.....

.....

.....

2. Tambua nomino katika sentensi zifuatazo kwa kupigia mistari kisha utaje ni za aina gani?

[Alama 5]

- a) Godoro zuri limenunuliwa:
- b) Kamau ameshinda:
- c) Kuchora kwake kunapendeza.:
- d) Maji yamemwagika.:
- e) Umati unaondoka.:

3. **Sentensi zifuatazo zinapatikana katika wakati gani?**

[Alama 3]

- a) Mtoto anasoma hadithi:
- b) Kaka alikula ugali kwa Samaki.
- c) Hali ya hewa itabadilika mwakani.

5. Tambua maagano na maamkuzi kutoka kwenye orodha ya maneno ifuatayo. [Alama 6]

HABARI?	ALAMSIKI?	SHIKAMOO?
KWAHERI?	BURIANI?	SABALKHERI

a) Maagano

b) Maamkuzi

.....

.....

.....

.....

6. Toa majibu ya maamkuzi na maagano yafuatayo.

[Alama 3]

a) Habari za utokako?

.....

.....

.....

